# Latra yasaka wasafirishaji wasiotoa tiketi mtandao, wanaozidisha abiria

**Na Kareny Masasy, Shinyanga**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) mkoani Shinyanga imeanza msako kwa watoa huduma za usafirishaji watakaobainika kukwepa kutoa tiketi za mtandao, wanaozidisha abiria katika kipindi hiki cha kuelekea sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Shinyanga, Denis Maghembe katika msako maalumu wa kukagua mabasi yanayotoa huduma ya kusafirisha abiria kwenda mikoani uliofanyika katika Kituo cha Mabasi cha Manyoni mkoani hapa, ukilenga kudhibiti uvunjifu wa sheria za usalama barabarani.

Maghembe alisema kwa mabasi yatakayobainika kukwepa kutoa tiketi mtandao, yatatozwa faini kwani wanaikosesha serikali mapato huku wakijua wazi kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria na kuwataka watoa huduma za usafiri kutojihusisha na ukiukwaji huo wa sheria.

"Katika msako wa leo (jana) makosa tuliyoyabaini ni mabasi madogo ya abiria matano yalizidisha abiria na kutotoa tiketi za mtandao na tumewatoza faini na wakirudia tutachukua hatua zaidi. Tumejipanga kudhibiti vitendo hivyo viovu na hatutaki ajali zisizo za lazima mwisho wa mwaka zijitokeze," alisema Maghembe.

Maghembe alisema kuwa msako huo unakwenda sambamba na kukagua watoa huduma ndani ya mabasi kama wamepatiwa mafunzo na kusajiliwa, kwani hilo ni takwa la kisheria ambapo utekelezaji wake ulikwishaanza kutekelezwa. Hivyo, ni lazima wamiliki wote wa mabasi wahakikishe watumishi wao wanakidhi vigezo hivyo.

Mmoja wa abiria, Peter Kisusi alisema ili kudhibiti mabasi kutojaza abiria ni lazima elimu itolewe kwa wakatisha tiketi, maana wao ndio sababu ya mabasi hayo kujaa kwani wanaweza kukata tiketi kwa abiria, huku wakijua wazi kuwa basi hilo limejaa.

"Nimetoka Simiyu naenda Mpanda. Nimekata tiketi, nimeambiwa nafasi zipo ila nimeigia kwenye gari naambiwa siti hakuna. Hii sio sawa, unakuta una shida unalazimika kusafiri kwa kusimama au kukaa chini, jambo ambalo linatweza utu wa mtu," alisema Kisusi.

Kondakta Doris Godfrey alisema kuwa LATRA wanatoa mafunzo ya namna ya kuwahudumia abiria, hivyo ni budi kila mwajiri akatekeleza takwa hilo la kisheria ili kuboresha utoaji wa huduma bora za usafirshaji hapa nchini.

CamScanner

pg 3

# Lori laparamia kijiweni, laua bodaboda watano

Na SELINA MATHEW, *Dodoma*

WATU watano wamefariki dunia, huku wengine wawili wakijeruhiwa baada ya lori la mchanga, kuacha njia, kisha kugonga kituo cha bodaboda, eneo la Makulu jijini hapa.

Waliofariki dunia ni Ishad Jaa (25), Michael Mkande (26), Adam Juma (27), Jumaa Ndafu (27) na Hafidhi Selemani (30).

Akithibitisha kutokea ajali hiyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gillus Hyera, alisema ajali ilitokea juzi saa 2:30 usiku katika eneo la Makulu.

"Lori namba T 824 EKS aina ya Fao Tipper, liliacha njia na kugonga bodaboda waliokuwa 'wamepaki' pembeni mwa barabara, ilisababisha madhara makubwa.

"Bodaboda watano walipoteza maisha na pikipiki zao kuharibiwa, pia gari hilo, liligonga ukuta wa nyumba na kuuvunja.

"Katika ajali hiyo, utingo wa lori aliyejulikana kwa jina moja la Alfonce alijeruhuwa," alisema Kamanda Hyera.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka dereva wa lori hilo am,baye baada ya ajali alitoroka eneo la tukio.

Kamanda huyo alitoa wito kwa madereva kuhakikisha wanaendesha vyombo vya moto kwa tahadhari kwa sababu vinaweza kukutana na changamoto.

"Pia, waendeshe kwa tahadhari kwa sababu, eneo hilo huwa lina msongamano wa watu wanaopita pembeni mwa barabara, wapo wanaoendesha shughuli zao, hivyo kuchukua tahadhari ni kwa usalama wake, chombo chake na watumiaji wa barabara hiyo.

"Tunasema hivyo kwa sababu, eneo hilo lina mteremko, ukianzia pale juu, hivyo likitoka juu kwa spidi kali hapa katikati akakutana na hali ya kushindwa kumudu," alibainisha.

**DC DODOMA MJINI**

Akizungumza katika eneo la tukio, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Jabir Shekimweri, alisema siyo tukio la kwanza kutokea eneo hilo, ni mara ya pili sasa, ukuta huo kubomoka kutokana na ajali.

"Hii ni mara ya pili, ukuta huu unaharibiwa na kujengwa kwa sababu ya ajali zinazotokea," alisema Shekimweri.

**OFISA HABARI WA HOSPITALI**

Ofisa Habari wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, Renatha Mzanje, alisema wamepokea miili ya bodaboda waliofariki katika ajali hiyo na majeruhi wanaendelea na matibabu.

"Ni kweli walipokelewa jana (juzi), usiku maiti tano. Majeruhi wanaendelea na matibabu, hali zao zinaendelea kuimarika," alisema Renatha.

**MASHUHUDA WANENA**

Masanja Joackim, ambaye alishuhudia ajali hiyo, alisema lori hilo, lilishindwa kukata kona katika mteremko, baada ya mpira wa breki kupasuka.

"Nilichosikia ni watu wakipiga kelele,

Inaendelea UK.5

CamScanner